# USHIRIKA

Na tuendelee kusimama, kwa muda kidogo tu, kwa ajili ya maombi, tunapoinamisha vichwa vyetu.

2 Baba yetu wa Mbinguni, tunapokukaribia Wewe, usiku wa leo, Bwana, katika wakati huu wa ushirika, tunakushukuru kwa ajili ya Damu ya Yesu Kristo, na kwa ajili ya wakati huu wa ushirika.

3 Sasa, mbele yangu kuna leso ambazo zimetumwa hapa, Bwana, kwenye huu mkutano mkubwa, zinawakilisha watu walio wahitaji. Nasi tunaambiwa katika Biblia ya kwamba walichukua kutoka kwenye mwili wa Mtakatifu Paulo leso na nguo, na pepo wachafu wakawatoka, na wagonjwa wakaponywa. Tunatambua ya kwamba sisi si Mtakatifu Paulo, bali Wewe ungali ni Mungu yeye yule, na umeandaa njia, leo, kwa kuwa Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele, tunaomba ya kwamba uwaponye watu hawa.

4 Pia jalia, kama mwandishi mmoja alivyosema, ya kwamba wakati Israeli walipozuiliwa na Bahari ya Chumvi wasiingie kwenye nchi ya ahadi, kwamba Mungu aliangalia chini kupitia ile Nguzo ya Moto kwa macho yenye hasira, nayo bahari ikaogopa na kufingirika nyuma, nao Israeli wakaendelea na safari, Mungu, ninaomba ya kwamba leso hizi zitakapowekwa juu ya mwili wa mgonjwa, naomba Mungu aangalie, si kupitia Nguzo ya Moto tu, bali kupitia Damu ya Mwanawe Mwenyewe, Ambaye alifanya. . .basi jalia ugonjwa urudi nyuma na kutoa nafasi kwa ajili ya nguvu za uponyaji za Kristo.

5 Bariki kongamano hili, Bwana, katika kumalizika kwake, usiku wa leo. Tunaomba ya kwamba utatutembelea tu kwa njia kuu, kama vile umekuwa ukifanya, na utupe baraka Zako. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

6 Mnaweza kuketi. Bwana awabariki. Nilichochewa *sana* na—na pongezi nilizopewa sasa hivi na Ndugu Carlson. Jinsi ningetaka kuchukua muda kusema mambo machache kuhusu hilo, lakini ninajua ya kwamba mmekuwa, leo, na kote katika mkutano huu mkubwa, kumekuwa na mahubiri mengi, na mahubiri mengi ya wahubiri mashuhuri ambao wamewazungumzia, nami ni—ninawathamini wote, nami najua mmechoka sasa, na mtakuwa mnaenda nyumbani baada ya kitambo kidogo, na labda kwenye makanisa yenu, kesho, basi si—sitachukua muda wenu mwingi. Lakini kama vile Ndugu Carlson, ta—tamshi zuri tu sana!

7 Jana usiku nilipoondoka hapa nilimkumbatia Joseph, nikasema, "Kwani nina shida gani?" Nilimwuliza mke wangu hivi majuzi, "Kwani mimi ni mwendawazimu?" Siwezi

kujizuia kusema mambo hayo. Kuna Msukumo ndani yangu unaoliendesha, wala si—siwezi kujizuia. Ni kitu fulani, ambacho, ninaangalia kote na juu ya Kanisa . . .

8 Alasiri ya leo, katika moteli ninayokaa, kulikuwa na kundi la watu waliokuja wakiwa wamelewa, na wanawake, na nyanya, huku wamevaa kaptura, na kuvaa kizinifu, na kunywa pombe, na kuvuta sigara, nami ni—nami nikawazia, "Mungu, kwa nini nizungumze na dada zangu jinsi nifanyavyo, huku sitaki kusema mambo hayo, lakini kwa nini nifanye hivyo, na kuangalia hapa?"

9 Na kwa utamu tu vivyo hivyo, si Sauti inayosikika, bali Kitu fulani ndani kikasema, "Sitaki watoto Wangu waonekane namna *hiyo*." Haya basi. Mnaona? Ninyi ni watu tofauti. Nilipomwona akisema, ama, kumsikia moyoni mwangu, "Siwataki watoto *Wangu*," hilo lilinifaidi, "Watoto *Wangu*." Ninalipenda Kanisa, Hilo ndilo Kristo alilifia, Kanisa. Nami ninaamini katika Kanisa, lakini baadhi ya mambo yanayoendelea Kanisani wakati sikuzote unahubiri dhidi yake, na kulielezea Neno, na halafu unaona Kanisa lingali linaendelea kupapasa-papasa katika hayo, ni . . .

10 Mnaona, kusema kweli, ninajua ninaitwa kila kitu kutoka malaika mkuu hadi ibilisi, mimi ni ndugu yenu, mimi ni ndugu yenu, na mambo hayo huenda yakasemwa kunihusu mimi, siwezi kuzuia yale yaliyosemwa, lazima niwe mwaminifu, mimi, nataka kusema kama Paulo, "Sikuliasi lile ono la Mbinguni," lililonijia kama mvulana, na tangu wakati huo Bwana ametenda kazi, nikimtumainia Mungu, imani katika Kristo.

11 Hapa majuma machache yaliyopita, mara ya mwisho nilipokuwa Chicago, hasa, nilikuwa na . . . Wafanyabiashara walikuwa wamefanya mandhari ndogo pamoja na wahudumu mbalimbali kote mjini, halafu ilinibidi nizungumze kwe—kwenye zamu ya kumalizia, se—sehemu yake ya mwisho, kwenye—kwenye kongamano la wahudumu. Nami nilikuwa nikijiandaa kwa ajili ya yubile kubwa ya mlo wa kiroho, nadhani ningeuita hivyo. Ndipo usiku mmoja, yapata siku tatu ama nne usiku hapo kabla ya ninii, kutukia, nilikuwa kwenye chumba cha hoteli, radi ilikuwa ikimulika, kulikuwa na dhoruba, nilikuwa ndio kwanza nitoke mkutanoni, ilikuwa yapata saa saba usiku, Yeye akasema, "Nenda dirishani." Kulikuwako na ile Nuru ikiangaza chumbani, ambayo mna picha yake, na mnajua habari zake. Kasema, "Sogea dirishani na usimame karibu na hiyo nafasi ya tatu."

12 Nami nikasimama pale, nikaangalia ng'ambo ya pili, Yeye akasema, "Wamekuwekea mtego, lakini usijali, nitakuwa pamoja nawe. Mwambie Bw. Carlson," *hapa*, "na mtu mwingine, atakayekuwa pamoja naye, ambaye atakuwa ni Tommy Hicks, hawatapata jumba hilo la mikutano wanalopangia, itakuwa mahali pengine penye chumba cha hudhurungi. Nao

watakapoingia, kutakuwako na mtu mweusi atakayeketi mkono wako wa kushoto." Ndipo akanionyesha mahali ambapo kila mtu atakuwa ameketi. Kasema, "Sasa, sema hilo, utakutana na Bw. Carlson, kesho, kwa ajili ya kiamshakinywa." Huyu *hapa* ameketi.

13 Basi humo chumbani, Roho Mtakatifu akaelezea kila sehemu yake. Ndipo mkutano huo, ambapo wangeufanyia, ulifutiliwa mbali, iliwabidi kuchukua chumba kingine, basi wakati wote walipoingia, kila mtu akaketi moja kwa moja mahali pao, huyu hapa Ndugu Carlson. Kamwe hasemi lolote ila lile lililo sahihi, kweli kabisa.

14 Ndipo nikaliambia shirika la wahudumu, "Ninajua mliyo nayo dhidi yangu, ni kuhusu mafundisho yangu juu ya Kristo. Sasa, niliwasikia mkijitambulisha kama Dk. *Nanii* na Dk. *Nanii*, hata sina elimu ya shule ya sekondari, lakini ninataka baadhi yenu nyote mnaosema mafundisho hayo si sahihi, kuninii, ambaye ni daktari, uchukue Biblia yako, uje hapa na kusimama karibu nami mbele ya wahudumu hawa, ama mwachane nami tangu sasa na kuendelea, mnaona." Hiyo ni kweli. "Iwapo ni tiketi ya posho kwenu, basi msijaribu kujadiliana nami, nina jambo moja, hilo ni kumpendeza Kristo na Neno Lake, na hilo ndilo kusudi langu maishani."

15 Basi marafiki, si rahisi unapowapenda watu, na hata hivyo inakubidi tu kuwakata vipande-vipande, humaanishi kufanya hivyo. Lakini mtu atakayehubiri kwa uvuvio anawezaje kusema lolote ila uvuvio unaomjia? Kama kamwe nikiwahi kusema jambo lolote ambalo ni kinyume cha Neno, basi ninyi nifahamisheni.

16 Bila shaka, mara nyingi miongoni mwa watu, huko nje ninapokuwa kwenye mifululizo ya mikutano mikubwa, sizungumzi lolote ila tu Fundisho kuu la kimsingi, la kiinjilisti. Wakati mwingine mimi hujaribu kunena dhidi ya dhambi, na kukemea mambo ninayoona watu wakifanya, huku wakijaribu kuishi kama walimwengu na bado wangali wanajifanya Mkristo. Ndilo jiwe kubwa sana la kujikwaa Kanisa limewahi kuwa nalo ni kama hilo, tunapaswa kuwa ama ndani au tuwe nje, ndivyo tulivyo, bali si kujifanya kitu fulani wakati sivyo tulivyo, na kwa hiyo inalifanya gumu sana.

17 Wakati fulani uliopita, rafiki yangu aliniandikia tu barua, kulikuwa na mtu aliyesimama pale karibu na rafiki huyu, kasema, "Ndugu Branham ni nabii wakati akiwa chini ya upako, lakini," kasema, "usisikilize fundisho lake, ni la uongo."

18 Sasa, mngeweza kuwazia mtu akisema hivyo? Ati nabii? Mbona, huyo ndiye anayejiliwa na Neno la Bwana! Walikuwa, wao ndio pekee waliokuwa na tafsiri ya Neno. Mimi si nabii, sidai kuwa nabii yeyote, lakini nasema, kama—kama mtu yeyote ambaye hangekubali kwamba Neno la Mungu ni la kweli, bila

kujali jinsi inavyotubidi kujikata . . . Hatuwezi kukata ninii ye—yetu . . . Hatuna budi kujichonga tupate kufanana na Neno la Mungu, hatuwezi kulichonga ninii le—letu, Neno la Mungu lilingane na yale tunayowazia, hatuna budi kudumu katika Neno.

19 Basi mtu mmoja alikuja si muda mrefu uliopita, kasema, "Fundisho hili, jambo hili unaloamini," kasema, "kama Malaika wa Bwana alikwambia hivyo, tutaliamini." Kundi la wahudumu.

Nikasema, "Ati Malaika wa Bwana? Kama akisema jambo lolote tofauti, nisingemwamini."

20 Unawezaje kujiwekea msingi juu ya tukio fulani, ama mhemuko fulani? Ibilisi anaweza kuiga mhemuko wowote unaoweza—unaoweza kujibunia. Nimeona upuuzi huu wote, nimewaona watu, nimewaona makafiri wakicheza katika roho, wakinena kwa lugha, na kunywa damu kutoka kwenye fuvu la kichwa cha mwanadamu, na kumwita ibilisi. Nimewaona watu wakipaza sauti, na kuingia, Waislamu, wanavichoma vidole vyao kwa vibanzi hata wasingeweza kuvihisi, wanachukua mkuki, na kujichoma usoni mwao namna *hiyo*, wakipaza sauti, wakipiga mayowe, wakimsifu mungu wao. Ati mnamwita huyo Mungu?

21 Nimewaona wakijichoma kwa ndoana za kuvulia samaki, matone ya maji yakining'inia *hivyo*, na kutembea juu ya moto wenye kina cha futi kumi na tano na upana wa futi nne namna *hiyo*, huku na huko, wasipate babuo la moto, wala hata harufu ya kuunguzwa. Ati mnamwita huyo Mungu? La hasha. Mungu ni Neno, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu," naye Neno angali ni Mungu. Tutahukumuje?

22 Mama yangu mwenyewe, akienda Mbinguni si muda mrefu uliopita, alisema, "Billy, umekuwa msaada wangu katika mambo ya kiroho, mimi, pia umenihudumia, umehakikisha ya kwamba sikuishi kwa njaa."

23 Nikasema, "Mama, sisi tuna msingi wa Kikatoliki, tunajua hilo, tukiwa Waairishi." Nikasema, "Nilipokuwa kijana mdogo na nilikuwa nimeuhisi wito wa Mungu," hatukuhudhuria kanisa lolote, si hata mmoja wetu, kamwe sikuwahi kuwa kanisani maishani mwangu, nadhani, mpaka nilipokuwa mtu mzima, nami nikasema, "mbona, nilihudhuria kanisa Katoliki, nao wakasema, 'Sisi ndio Kanisa.' Ninashuka kwenda kwa Walutheri, wanasema, 'Sisi ndio Kanisa.' Kule kwa Wabaptisti, 'Sisi ndio Kanisa.'"

24 Vema, Kanisa ni lipi? Kuna mia tisa na *kitu* yao, hakuna mtu anayeweza kuwekea msingi imani juu ya hilo; hakuna mtu anayeweza kuwekea imani yake msingi juu ya mhemuko. Kuna Moja tu lililo la kweli, na hilo ni Neno la Mungu, "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita."

25 Hawa alifasiri vibaya tu, ama, Shetani alimfasiria Hawa, sehemu moja tu ndogo ya Neno la Mungu, kitu kidogo tu, nacho kimesababisha matatizo haya yote. Hiyo ni kweli? Kila kifo, kila—kila mtoto mchanga, kila mtoto mchanga mwenye kichwa klichojawa maji, kila mtu aliyelemaa, kila—kila kifo, kila eneo la makaburi, na kila kitu, ilikuwa ni kwa mtu mmoja kutokuamini tu Neno la Mungu kwa pindo moja dogo. Na kama Mungu asingeliacha lipite wakati huo, ni zaidi sana vipi sasa? Tutakuja kwenye Neno, la sivyo hatutakuja hata kidogo. Hiyo ni kweli.

26 Kwa hiyo unaweza kuwazia, watu wenye upendo, watu wa kupendeza, na jinsi inavyohitajika kusimama pale na kutofikiria yale utakayosema, na kumwona Roho akiyakemea sana mambo hayo, lakini hata hivyo, ile faraja ya Yeye kuwa pamoja nawe kumwona Yeye akija, kuonyesha mambo. Ninaweza kuchukua . . . Mtu yeyote anayefikiri nilikuwa mpiga ramli, mtabiri, mnajua hiyo ndiyo sababu hasa ya wao kumwua Yesu? Jambo lile lile, maana Yeye aliyatambua mawazo yao na kadhalika.

27 Kama ningeyasoma mawazo hapa jana usiku, ninge—ningekuwa na ninii, ninii sana . . . Kama Roho Mtakatifu angeniruhusu kuzungumza jana usiku juu ya mambo kama hayo yaliyokuwa yakiendelea, mngalinifukuza nchini. Watu wanakupigapiga mgongoni na kusema, "Ndugu," na kuwazia wewe ni mpiga ramli? Hivi hamfikirii najua hilo? Siwezi kuwa na Roho wa Mungu bila kujua hilo, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya; nyingi kuliko hizi atazifanya, Mimi naenda kwa Baba Yangu." Mnaona ninalomaanisha?

Na tuombe.

28 Baba wa Mbinguni, jalia Roho Mtakatifu sasa anene nasi katika maneno haya machache yanayofuata. Mungu, ninaomba ya kwamba hakutakuwako na hata mmoja atakayekosekana kwenye ile Siku ya Hukumu, kwamba sote tutakuwako, na sote tufunikwe na Damu ya Mwana wa Mungu. Utusamehe makosa yetu. Tunakusikia, ulisema wakati mmoja, ulipokuwa ukitufundisha kuomba, Nawe ukafikia mahali pale, "Utusamehe deni zetu kama tunavyowasamehe wadeni wetu," ndipo ukasimama na kusema, "Kama ninyi, kutoka moyoni mwenu, hamtamsamehe kila mtu kosa lake, wala Baba yenu wa Mbinguni hatawasamehe ninyi," kwa hiyo tunaona mahali tulipo.

29 Mungu, ninatumaini kuishi kuona siku ambayo ninaweza kuliona Kanisa la Mungu aliye hai wote wamejipanga kama jeshi moja kuu la Kristo, wote wamefunikwa na Damu, kila dada na ndugu mtakatifu, wakisonga mbele katika nguvu za Neno la Mungu. Ulisema utarudisha yote yaliyoliwa na parare, na nzige, na madumadu, ninaamini Wewe utafanya hivyo, Bwana.

Ninashikilia kwamba Wewe utafanya hivyo, nami natumaini kuliona katika wakati wangu, kama sivyo, nitapanda Mbegu ya Neno Lako, ndipo basi Roho Mtakatifu atakaposhuka, Yeye ataninii . . .

30 Tunawajua wenye haki, mvua huwanyea wenye haki na wasio haki, mvua ile ile inayotia ngano maji, hutia maji magugu, lakini, Baba Mungu, jalia katika maisha yetu tusipande chochote ila Mbegu halisi ya Mungu, kwa hiyo wakati Roho atakapokuja na kushuka juu Yake, jalia lilete uzao wa Yesu Kristo, ukiwa mwana ama binti wa Kristo. Ninaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

31 Mungu awabariki sana nyote. Baraka zangu pamoja nanyi, amani yangu juu yenu. Nami sininii . . . Ninatumaini na kuamini ya kwamba siku moja katika ninii nyingine, kama sio tena katika nchi hii, katika Nchi ile ijayo wakati tutakapoitwa kumkabili Kristo, kwamba parapanda italia, waliokufa katika Kristo watafufuka, kwamba pamoja, kundi moja kuu, tutaenda kumlaki.

32 Ninataka kuzungumza tu kwa, nina saa ya mkono hapa, ninaweza kuweka na kuifanya dakika thelathini kamili, na hiyo itakuwa ni saa nne kamili, na Mungu akipenda, nitamalizia papo hapo. Kwa muda mfupi tu wa wakati wenu, kama mtautoa, kidogo tu.

33 Sasa, kesho alasiri, kwenu ninyi watu kutoka nje ya Chicago, waleteni wagonjwa wenu na wanaoteseka, kesho alasiri, huko Mather kutakuwako, ibada ya uponyaji. Hilo ni sawa, Ndugu Carlson, sivyo? Nilimwuliza Ndugu Joseph kama ingekuwa sawa, akasema alikuwa na hakika ingekuwa, kwa hiyo hilo ni sawa. Halafu Jumatatu ni mkutano wa kimishenari kwa ajili ya Ndugu Joseph, maskini jamaa huyu mwema ambaye sisi sote tunampenda.

34 Nikizungumza tu na ndugu fulani hapa ambaye, ninaamini alikuwa amenipeleka kwa Ndugu *Hegre* wakati huo, Hegre, nilipopata barua kali sana kutoka kwake, naye Bwana akatupa hayo Maneno makuu, nami nafikiri labda arobaini au zaidi walimpokea Roho Mtakatifu huko nje kwenye chuo cha Kilutheri. Ungeweza kuwazia jambo hilo? Lakini wakati alipokuja, pia, alidhani ilikuwa ni mtabiri, kitu kilichopigwa msasa, lakini alipokuwa mwaminifu vya kutosha kuketi chini kwenye Neno la Mungu, ndipo lilimjia, na hilo likaleta tofauti.

35 Sasa, nitasoma kutoka katika Yohana Mtakatifu, mlango wa kwanza wa, si Yohana Mtakatifu, samahani, wa Yohana wa Kwanza, mlango wa kwanza, 1:7. Hebu sote tusome kifungu hiki:

> *Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu Kristo, Mwanawe, yatusafisha dhambi yote.*

36 Ninataka kuzungumza kwa muda mfupi tu juu ya wazo la *Ushirika*. Basi hili likiwa ni mkutano mkubwa, sote tunajua ya kwamba mkutano ni wakati wa ushirika. Nasi tunanii... Ninapenda ushirika, ninapenda kuja kwenye mkutano wa ushirika ambapo tunaweza kuwa na ushirika.

37 Na kama mtaniwia radhi, baada ya kusoma somo langu, kwamba ni—nitoe tamshi kwa ndu—ndugu anayeketi hapa, Ndugu Tommy Nickel. Nina furaha sana, wakati ulipochapisha makala hiyo, ama—ama, katika, ninii yenu, *Sauti* ya Wafanyabiashara, kuhusu ono la kwenda Mbinguni, ulililiweka jinsi hasa lilivyokuwa. Asante, Ndugu Tommy. Mungu akubariki kwa hilo.

38 Sasa, juu ya *Ushirika*, kwenye ushirika, kila mtu anautaka. Usiku wa leo, pale kwenye moteli, walikuwa na ushirika. Ilikuwa ni kitu gani? Kunywa pombe. Walikuwa, walienda wakanunua chupa zingine zaidi na pombe ng'ambo kwenye vilabu vya pombe, nao hawa hapa wote, akina nyanya na babu, wakinywa pombe na kupiga makelele, mambo ya utovu wa uadilifu kabisa ilinibidi kuninii, katika chumba chenye joto, ilibidi nivute madirisha na kuyafunga, nisije nikasikia hayo makelele makubwa. Na inaonekana kwangu kama, kama tunaishi katika taifa la Kikristo, hilo hata halipaswi kuruhusiwa. Lakini nawaambia jambo moja, hebu anza kupiga mayowe na kupaza sauti, na uangalie hilo litadumu muda gani, kutakuwa na jambo fulani litakalosemwa kuhusu hilo upesi sana, hata hivyo, tuko katika "Marekani ya Kikristo."

39 Nilisimama chumbani, nikaenda, leo, kula chakula cha kutwa mahali padogo. Kama nikiwahi kuja hapa tena, nitakula chakula cha kutwa *hapa*, kama ninaweza kuingia na kujipatia chumba mahali fulani. Nilienda kula chakula cha kutwa mahali padogo, na kusema kweli walikuwa na ile bugibugi, mwajua, roki. Mimi ni mmishenari. Nimekuja... Nimekuwa huko ndani, huko mbali sana kwa Wahotentoti, na huko chini kwenye misitu ya Afrika, nilisikia hiyo huko nyuma, lakini kamwe nisingefikiria ningeisikia Marekani. Basi hiyo hapo ikiendelea, na hao wote wakiendelea, ikanikera kabisa, ndipo mimi na Billy tukasimama, tukaondoka, tukaenda mahali pengine. Na—nao hawakuwa na wowote mle ndani, nikasema, "Chungulia ndani, na iwapo wana moja ya maskini hayo masanduku ya santuri, hatutaingia, tutaachana nacho tu."

40 Nilipeleka familia yangu katika moja, wakati mmoja tukisafiri, walikuwa wameifungulia, nikaenda mle, nikasema, "Bwana, mimi ni mmishenari, nami ninahitaji kila senti niliyo nayo, lakini nina familia yangu, nasi sote tuna njaa, tumekuwa yapata saa tatu tukijaribu kupata mahali pa kula. Nitakupa noti ya dola tano kama utazima plagi ile pale, mpaka nitakapomaliza kula."

41 Ilimfanya ajionee aibu sana, kasema, "Weka tu dola zako tano. Kama una ujasiri kiasi hicho," akasema, "achana tu nayo." Kwa hiyo ndivyo hivyo. Loo, "Marekani ya Kikristo," bila shaka, naam, "Marekani ya Kikristo."

42 Tulijaribu kila kitu. Wana ushirika kwa vitu kama hivyo. Kunguru wana ushirika juu ya mzoga uliokufa, bali hua hula chakula cha hua, wana ushirika katika shamba la ngano. Na kwa hiyo inategemea kile ninii yako. . . kile ulicho. Hua hawezi, sasa hawezi kushirikiana na kunguru na nderi, kwa sababu yeye hana nyongo, hakuna uchungu juu yake, asingeweza kuula, ungemwua. Naye Mkristo hawezi kufanya ushirika namna hiyo, ingemwua Roho yeye yule aliyekuwa ndani yake, ingemhuzunisha Roho Mtakatifu Naye angeondoka.

43 Sasa, tunajaribu kufanya ushirika na mataifa, tunatumia mabilioni ya dola, tukiyapa mataifa ya kigeni tufanye ushirika, huku ukomunisti ukienea kote nchini vivyo hivyo. Mnaona?

44 Hapa si muda mrefu uliopita, mbona, vema, tulikuwa na vita, na baadhi ya hivyo vitu, tulivyorushiwa tena vilitengenezwa Marekani. Mnaona, wakijaribu kuwapelekea vitu, na mambo kama hayo, nao wanaturushia tena. Huwezi kupata ushirika namna hiyo, kamwe huwezi.

45 Sasa, tumejaribu, basi, kuwaelimisha watu kufanya ushirika. Hakuna njia ya kuwaelimisha watu kufanya ushirika, unaenda mbali zaidi wakati wote. Kanisa lilipoteza haki zake za mzaliwa wa kwanza wakati lilipochukua elimu, badala ya wokovu, kujaribu kuwaleta watu wapate kumjua Kristo. Walijaribu kufanya dhehebu wapate ushirika, hamwezi kufanya hivyo, kwa sababu mnaweka mpaka, mnamwondosha huyo jamaa mwingine, hamwezi kufanya hivyo. Hakuna njia ya—ya kufanya ushirika katika madhehebu. Kamwe hutaweza kufanya hivyo, maana kila dhehebu, Baraza hili la Makanisa Ulimwenguni, mbona, wanapigana wenyewe kwa wenyewe, wanajikata koo.

46 Wanawezaje kupata ushirika, wakati watu mle ndani hata hawamwamini Mungu? Makafiri na chochote kile! Unawezaje. . .? Yesu alisema, "Watu wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipokuwa wamepatana?" Mnawezaje kufanya hivyo? Kuna njia moja tu unayoweza kutembea na mtu mwingine, hapo ni wakati umekubaliana naye. Kwa hiyo utakatiliaje katika madhehebu na kadhalika, na kufanya mapatano, wakati mmoja anapojitenga na mwingine?

47 Na hata hivyo, Mungu anatutaka tufanye ushirika. Kuna kitu ndani yake cha kufanya ushirika. Mwanadamu sikuzote ametaka kufanya hivyo, bali daima amejaribu kufanikisha kwa maarifa yake mwenyewe jinsi ya kuuleta, wala kamwe hataweza kufanikisha.

48 Kuna mahali pamoja tu pa ushirika halisi, na hapo ni chini ya damu iliyomwagika ya asiye na hatia. Hivyo ndivyo tu tunavyoweza kuufanya. "Tungekuwa na ushirika kama kila kanisa lingekuwa la Kilutheri." "Kama kila kanisa lingekuwa la Kibaptisti," ama kadhalika, "tungekuwa na ushirika chini ya haki za kimadhehebu." Lakini sisi, tunaosoma Biblia, tunajua ya kwamba mambo haya yanatufanya kutokubaliana.

49 Sasa, jambo pekee tunaloweza kuwa na ushirika chini yake, ni kama tulivyoketi hapa usiku wa leo, Wamethodisti, Wabaptisti, Walutheri, Presbiteri, ama lolote lile, tunapokuwa chini ya damu iliyomwagika ya asiye na hatia, hayo yalikuwa ndiyo matakwa ya Mungu, wala Mungu kamwe habadilishi mpango Wake. Mungu anapofanya uamuzi mara ya kwanza, hana budi kudumu na uamuzi huo milele.

50 Sasa, Yeye hana kikomo. Sisi—sisi si wasio na kikomo, sisi ni—sisi ni wanadamu, kwa hiyo basi sisi tuna kikomo, kwa hiyo hatuwezi kuwa—kuwa wasio na kikomo. Kwa hiyo basi tunafanya ahadi, ukifanya ahadi, inakubidi kuzivunja. Unafanya jambo fulani leo, na kesho unajua zaidi kulihusu, kwa hiyo unaweza kulifanya vizuri zaidi kesho. Mwaka ujao bado unaweza kulifanya vizuri zaidi kuliko ulivyofanya siku hiyo, kwa sababu unajifunza mengi zaidi kulihusu, maana sisi tuna kikomo, tumefungwa kwa—kwa viwango hivi vidogo vitatu tunamoishi.

51 Lakini Mungu hana kikomo, kwa hiyo, Mungu anaweza kunena mara moja na hivyo, uamuzi Wake ni mkamilifu, wala hauwezi kubadilika, hiyo ndiyo sababu:

> Imani yangu haijajengwa juu ya chochote pungufu
> Ya Damu na haki ya Yesu;
> Kila kitu karibu na nafsi yangu kikitoweka,
> Basi Yeye ndiye tumaini langu lote na nanga yangu.
>
> Kwa kuwa juu ya Kristo, Mwamba imara, ninasimama;
> Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.

52 Naye Kristo ni Neno, Yeye ni Neno. Juu ya . . . Yeye alisema ya kwamba "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe." Hakuna hata Neno Lake moja linaloweza kushindwa, kwa sababu ni Neno la Mungu. Huwezi . . . Katika Kitabu cha mwisho, cha Ufunuo, lilisema, "Yeyote atakayeondoa Neno moja kutoka kwa Hili, ama kuongeza neno moja Kwake, huyo ataondolewa, sehemu yake katika Kitabu cha Uzima."

53 Kwa hiyo, kanuni yoyote ya imani, kitu kingine chochote ambacho kingeongeza chochote kwenye Neno la Mungu, ama kuondoa chochote Kwake, ni mauti kufanya hivyo, kama ilivyokuwa kwa Hawa hapo mwanzo. Ni hukumu ya

kifo kuchukua au kuongeza, lichukue tu jinsi linavyosema. Biblia inasema, "Si la kufasiriwa apendavyo mtu yeyote." Tayari limefasiriwa, lisome tu na uliamini. Mungu huliangalia Neno Lake apate kulitimiza, kwa hiyo ni Neno Lake, kile tunachopaswa kusimama juu yake.

54 Sasa, mahali pekee, kwa hiyo kuliamini Neno Lake, mahali pekee, chini ya Damu iliyomwagika ndipo mahali pa ushirika, ambapo kila mtu anaweza kukusanyika na kujisikia sawa, kwa sababu ni chini ya mahali pamoja pa Damu iliyomwagika. Sasa, kuweka imani yako juu ya kitu kingine chochote, mbali na Neno la Mungu, ni mchanga udidimiao. Haidhuru ni nini, ingali ni mchanga udidimiao. Haina budi kuwa ni Neno. Hiyo ni kweli. Tunaamini hilo.

55 Hiyo ndiyo sababu nina imani ya kuamini jambo hilo, kila kitu ambacho Mungu aliahidi. Sasa, nasema Mungu anaweza kufanya mambo ambayo hayajaandikwa katika Neno, hiyo ni kweli, lakini maada-. . . Sina budi kushangaa kuhusu hilo, lakini maadamu Yeye ananipa kile alichoahidi *Humu*, nitaridhika tu na yale aliyoahidi, ndipo nina hakika ya kuwa sawa. Dumu na Neno Lake, Neno Lake haliwezi kubadilika, kwa maana kama anaweza kubadilika, basi Mungu anaweza kubadilika, kama Neno linaweza kubadilika, kama Neno linahitaji kubadilishwa, basi Mungu si Mungu.

56 Kama Mungu alikutana na mwanadamu, na juu ya msingi wa imani yake, chini ya damu iliyomwagika, akamwokoa mtu wa kwanza, Adamu, hana budi kubaki milele chini ya mpango ule ule, kama hakufanya hivyo, alifanya kosa alipotoa uamuzi Wake wa kwanza. Kama Mungu alimwokoa mwanadamu, na njia pekee aliyomwokoa ilikuwa ni kwa damu iliyomwagika ya mwana-kondoo asiye na hatia, kama huo ndio msingi ambao Mungu aliamua kumwokolea mwanadamu, chochote, kama akiwahi kuubadilisha uwe kanuni ya imani ya mtu fulani, ama kanisa, ama fundisho fulani la sharti, basi Mungu alifanya uamuzi mbaya katika bustani ya Edeni, kwa kuwa mtu wa kwanza aliyepata kumwokoa, alimwokoa juu ya msingi wa imani yake katika damu iliyomwagika ya mwana-kondoo asiye na hatia, hapo ndipo mahali pekee ambapo angeweza kuja.

57 Mungu alichagua mahali, akawaita Adamu na Hawa, kisha akamwaga damu ya asiye na hatia na kuwafunika na vitu vya huyu asiye na hatia, pamoja na damu juu yao. Huo ulikuwa ndio msingi ambao mtu huyo angeweza kuzungumza na Mungu, na kusikia Neno Lake, na kupata Neno Lake, ilikuwa ni chini ya damu iliyomwagika.

58 Na njia pekee ambayo wanadamu, ama makanisa, ama watu watawahi kujua ukweli halisi kumhusu Mungu, ni kuja chini ya Damu iliyomwagika ya Mtu asiye na hatia waingie katika Uwepo Wake, ndipo Roho anayekuja juu yako atashuhudia ya

kwamba Neno hili ni kweli, kila Neno Lake, wala halihitaji kusahihishwa mahali popote. Hiyo ni kweli. Ha—halina budi kubaki hivyo, maana Yeye ni Mungu, na uamuzi Wake hauna budi kuwa mkamilifu, na mkamilifu milele.

Hebu tupitie jambo hilo, kwa dakika chache tu. Muda si muda mwajua dakika zangu thelathini zitakwisha wala sitakuwa nimeanza.

59 Sasa, na chini ya Damu iliyomwagika . . . Sasa, tunatambua ya kwamba Kitabu cha kale sana kuliko vyote katika Biblia ni Ayubu, Kitabu cha kale kuliko vyote kilichoandikwa. Kiliandikwa kabla Musa hajaandika Mwanzo, inasemekana kiliandikwa kabla ya Musa kuandika Mwanzo, hasa.

60 Sasa, angalieni, Ayubu, mtu mwenye haki, mcha Mungu, kila kitu dhidi yake siku moja, Shetani aliwazia kumfanya amkane Mungu. Na alipofanya hivyo, Ayubu . . . Ninapenda kusoma Ayubu. Watu wengi wanasema ni kitendawili, sivyo, ni Neno la Mungu. Yesu alirejea kwa Ayubu kuhusu, "Hivi hamjasikia habari ya subira?"

61 Haidhuru ni kitu gani kilichokuwa kikiendelea, jinsi alivyoteswa, jinsi alivyoitwa kwamba alikuwa, katika njia mbaya, Ayubu alidumu imara katika Neno, napenda hilo. Akasema, "Labda watoto wangu wametenda dhambi, nitatoa dhabihu kwa ajili yao."

62 Sasa, jambo pekee mtu huyo alilojua lilikuwa ni sadaka ya kuteketezwa, hiyo ilikuwa matakwa ya Mungu. Basi watu wengi wanafikiri, wakati mwingine, ati kwa sababu maafa humpata Mkristo, "Loo, aliyaacha mapenzi ya Mungu. Waliondoka kanisani, wakatoka nje . . . " Wakati mwingine hilo si kweli, kwa sababu Mungu humrudi kila mwana amjiaye, Yeye humtakasa, na kumsafisha, na kumjaribu, kuona kama atasimama, hivyo ndivyo alivyokuwa akifanya katika wakati wa Ayubu.

63 Nilihubiri juu ya Ayubu wakati mmoja kwa yapata miezi sita nilipokuwa mchungaji, kulikuwa na mama aliyekuwa mwaminifu vya kutosha, nilimpeleka kwenye lundo hilo la majivu, ameketi pale, mwajua, amejaa majipu na kipande cha kigae akiyakuna majipu yake, ndipo mama mmoja akasema, "Ndugu Branham, kweli utapata kumwondosha Ayubu kwenye lundo hilo la majivu?"

64 Yapata Jumapili tatu, lakini nilikuwa nikilijengea nipate kulifanikisha: huyo hapo, alikuwa nabii, alikuwa ni mtiwa mafuta wa Mungu, na jambo pekee mtu huyo alilojua kufanya lilikuwa ni kudumu na Neno, hivyo tu. Walikuja nao wakasema, "Ayubu, unajua umefanya kosa. Angalia kile kilichokupata, kila mtu amekupa kisogo, na hapa marafiki zako wameondoka na wote, na jambo pekee unaloweza kufanya ni kuketi hapa nje, angalia, wewe ni mnyonge mwenye mashaka sana, huku umejaa majipu na kila kitu, halafu angalia hali yako." Lakini

Ayubu alisema hakuwa ametenda dhambi, kwa sababu alikuwa anakuja kwa njia iliyowekwa na Mungu chini ya damu iliyomwagika.

65 Ndipo Mungu anawajibika kwa mtu atakayesimama namna hiyo. Alimwacha aende moja kwa moja hata kwa mtu wa mwisho, hata kwa mkewe, alijitokeza na kusema, "Ayubu, kwa nini usimkufuru Mungu upate kufa?" Wazia tu, mke wake mwenyewe alimgeuka. Na kwa sababu mtu fulani atatugeuka na kuwazia kwamba sisi ni wa kuchekesha na wa kipekee... Watu wote wa Mungu ni wa kuchekesha na wa kipekee kwa ulimwengu. Hakika, ndivyo walivyo, "Ninyi ni watu wa kipekee, ukuhani wa kifalme, mkimtolea Mungu dhabihu, matunda ya midomo yenu mkilisifu Jina Lake."

66 Sasa, tunaona ya kwamba hata mke wa Ayubu alimgeuka, akampa kisogo na kusema, "Kwa nini usimkufuru Mungu upate kufa?" Kwa maneno mengine, "Unaonekana mwenye mashaka. Kwa nini usimkufuru tu Mungu upate kufa?"

Akasema, "Wewe wanena kama mwanamke mpumbavu."

67 Sasa, kamwe hakumwita mpumbavu, alisema alizungumza kama mmoja, kamwe hakusema alikuwa mpumbavu. Kwa kweli, hebu, nilisahihishe hili: Wakati mwingine ninapowaita ninyi akina dada, sisemi ninyi ni wa kilimwengu, lakini wakati mwingine mnafanana nao. Kwa hiyo si—si—sisemi ungefanya makosa, lakini wakati mwingine unavalia kama—kama, inaonekana hivyo, unaona. Kwa hiyo Ayubu akamwambia mke wake...Sitaingilia hilo. Ayubu alimwambia mkewe, kasema, "Wewe wanena kama mwanamke mpumbavu."

68 Na baada ya kitambo kidogo...Loo, Mungu daima ni mwaminifu tunapokuja kwa njia iliyowekwa na Mungu. Ayubu akasema, "Nimefanya maungamo yangu. Nimeiteketeza sadaka." Hivyo ndivyo hasa Mungu alivyohitaji. Alimwabudu Mungu chini ya damu iliyomwagika, na kwa ghafla Roho akamshukia huyo nabii, ndipo ngurumo zikanguruma, na radi zikamulika, naye akasema, "Ninajua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho, ingawa baada ya mabuu ya ngozi kuuangamiza mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu, ambaye nitamwona mimi mwenyewe." Mnaona, chini ya damu!

69 Hao hapo hao wengine wameketi mbali sana kama chochote kile, lakini Ayubu ameketi chini ya damu pamoja na Neno. Jambo ndilo hilo, chini ya Damu pamoja na Neno. Haidhuru kunakuwa giza kiasi gani, endelea tu kwenda mbele. Shikilia Neno la Mungu lisilobadilika, shuka moja kwa moja, kama ukilishikilia Neno, umeushika mkono Wake, endelea kushuka chini.

70 Ndipo basi, yeye akiwa ni nabii, umeme ulimulika naye akaona ono la kuja kwa Mungu, alijua ya kwamba mabuu

ya ngozi yake yangeuangamiza mwili wake, lakini akasema, "Hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu, ambaye nitamwona mwenyewe, macho yangu yatamwona, wala si mwingine. Kwa kuwa hatukuleta chochote humu ulimwenguni, ni hakika hatuondoi chochote. Bwana alitoa, Bwana ametwaa; libarikiwe Jina la Bwana." Alidumu kwenye hiyo damu iliyomwagika pamoja na Neno, ile ahadi. Alikuwa wa kiroho, alikuwa nabii. Ilionekana kana kwamba Mungu alimpa kisogo, bali ni kujaribu tu kuona kama angedumu pamoja na Neno.

71 Sote tunajaribiwa, kila Mkristo, kila mwana, kila mwana amjiaye Mungu hujaribiwa kwa Neno, aone kama utakuwa mwaminifu Kwake. Wakati shindano la kuamua litakapokuja, utafanya uamuzi gani? Jambo ndilo hilo. Naye asiyeweza kustahimili kurudiwa, bali anaendelea na ulimwengu, yeye ni mwana haramu, wala si mwana au binti wa Mungu, la hasha.

72 Sasa, bali yeye aliye na nia ya kiroho hulishika Neno, anajilainisha Nalo, naye Roho anashuka chini ya Damu iliyomwagika na kumchukua mtu huyo.

73 Israeli walikuwa na mahali pamoja pa kukutania kwa ajili ya ushirika, mahali pamoja tu ambapo Israeli wangeweza kukutana na Mungu, hapo palikuwa ni chini ya damu iliyomwagika. Hakuna mahali pengine ambapo Mungu alikutana nao, ila chini ya damu iliyomwagika.

74 Sasa, tutaingia katika Hesabu mlango wa 19 kwa muda kidogo tu kulinukuu, hatutakuwa na wakati wa kulisoma, bali kulinukuu tu. Tunaona katika Hesabu 19 tunaona jambo hili, ya kwamba Mungu aliwaambia wana wa Israeli safarini mwao, kasema, "Nileteeni ndama mwekundu ambaye hajatiwa nira." Hiyo ni nini? Hilo linamaanisha jambo fulani.

75 Kama tungalikuwa na wakati tungeweza kuingia katika mifano hiyo, ndama mwekundu, lazima awe mwekundu, hana doa, mwekundu. Nyekundu ni rangi mbaya katika maana moja ya neno, lakini nyekundu ni rangi ya upatanisho. Hivi ulipata kujua, kisayansi, nyekundu kupitia nyekundu inaonekana nyeupe? Vema. Nyekundu kupitia nyekundu, ukiangalia nyekundu kupitia nyekundu, inaonekana nyeupe. "Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu kama bendera," bali wakati Mungu anapoziangalia kupitia Da—Damu iliyomwagika ya Mwanawe, nyinyi ni weupe kama theluji, nyekundu kupitia nyekundu, hakuna rangi nyingine inayofanya hivyo, nyekundu kupitia nyekundu inaonekana nyeupe, na hivyo ndivyo Mungu anavyokuangalia. Ingawa wewe, haidhuru wewe ni nani, kama ukija chini ya Damu iliyomwagika, Mungu hakuoni, bali Yeye huangalia kupitia kwa Damu, na dhambi zako zijapokua ni *nyingi sana*, hata hivyo unaonekana mweupe kama yungiyungi Kwake.

76 Ndama mwekundu asiye na madoa juu yake, hapaswi kamwe kuwa na nira shingoni mwake. Ningeweza kulipua hilo vipande-vipande sasa hivi, hajafungwa nira na chochote, hiyo ni kweli, hakuna dhehebu lisiloamini, yeye anakaa huru. Basi alikuwa awe nini? Dhabihu. Ndipo alipaswa ateketezwe kwa moto, auawe wakati wa jioni, kwenye, si asubuhi, jioni, na halafu anapaswa kuteketezwa, na majivu yake yalikuwa yawekwe kando kwa ajili ya maji ya farakano. Loo, ni mandhari nzuri jinsi gani hii, laiti tungaliweza kuingia ndani yake, jinsi yale maji, ama, majivu yalipaswa kutiwa, yalivyofanywa maji ya farakano. Kwa hiyo, basi walikuwa wachukue damu yake na kufanya milia saba juu ya mlango ambapo uliingia katika kusanyiko, kutoka uani ukaingia katika kusanyiko, ukaingia katika mahali patakatifu, na halafu Roho alikuwa katika Patakatifu pa patakatifu.

77 Angalieni, sasa, ni picha nzuri jinsi gani hapa! Natumaini dakika hizi tano ama sita zijazo mnaweza kulishika. Angalia, Patakatifu pa patakatifu, na njia ya kukaribia iliyoandaliwa kwa ajili ya mtu mchafu, walikuwa na taratibu fulani ambazo hawana budi kupitia. Wa kwanza, aliye mchafu hana budi kuja kwenye nyua za nje, na hapo anyunyiziwe maji ya farakano. Maji ya farakano ni nini? Biblia inatwambia ya kwamba tunaoshwa kwa maji ya Neno la farakano. Kwa hiyo, Neno hututenganisha na kutokuamini kwetu. Kanuni ya imani ingewezaje kufanya hivyo? Ni Neno, Neno linatutenganisha, Hilo ndilo Kitu kinachotufanya kujua ya kwamba tumekosea. Kama ulienda kwenye kanisa lililosema, "Ni sawa kufanya jambo *hili*," kisha ukaenda huku, na kusema, huku, "na kufanya *hilo*. . . " Njoo kwenye Neno; Neno ndilo linalotutenganisha.

78 Na sasa, angalieni, jambo lingine. Natumaini mtanisamehe kama nikipita wakati huu. Angalieni, jambo lingine. Ni nzuri sana kuliachilia. Yule aliyenyunyizia maji haya ya utengano hana budi kuwa na mikono safi, na hayo lazima yawekwe mahali safi. Maji ya farakano hayawezi kukaa mahali pachafu, lazima yawekwe mahali safi.

79 Nyua za nje, ni kitu gani? Mwenye dhambi anayekuja na kulisikia Neno na kujenga imani ndani yake ya kwamba ni Mungu. "Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu." Sasa, tunajaribu kufanya nini? Kuingia katika ushirika. Sasa, huyo mtu alilisikia Neno, akaliamini Neno, naye basi akanyunyiziwa maji ya farakano, hata hivyo hakuwa katika ushirika, la, bwana. Sasa, ninyi wa kimsingi, ninawatakeni mwangalie hili: Yeye bado hakuwa katika ushirika.

80 Kumbukeni, wakati Israeli walipopanda kutoka Misri, Moabu alikutana naye wala wasingemruhusu kufanya uamsho nchini mwake, hakukuwako na ushirikiano. Nao Moabu walimwamini Mungu yeye yule ambaye Israeli walimwamini. Walienda wakamleta askofu wao huko juu, Balaki, wakamleta

huko chini, naye alikuwa wa kimsingi tu kama Israeli walivyokuwa, Israeli, huyo mzururaji, hana mahali pa kwenda. Taifa hili kuu, lenye utaratibu hapa, pamoja, wakawaleta watu wao mashuhuri huko nje kulaani kundi hilo la waasi, walisema, wakija kule.

81 Walisahau ya kwamba kundi hili la watu, ambao hawakuwa na mahali pa kwenda, bali walikuwa ni wazururaji na wasafiri na wageni, walikosa kuiona hiyo Nguzo ya Moto iliyowatangulia, walikosa kumwona yule nyoka wa shaba, na Mwamba ule uliopigwa ukiwafuata, ingawa walikuwa wamefanya kosa.

82 Balaamu aliwazia, "Hakika, mimi nikiwa mtu wa kimsingi, hakika nitafanya hivyo." Naye akajenga madhabahu saba, hizo ndizo Mungu alizohitaji, namba kamilifu. Akaweka fahali saba safi, sawasawa kabisa na wale Israeli walikuwa nao. Madhabahu saba ndizo Israeli walikuwa nazo, vinara vya taa saba, na kadhalika, hesabu kamilifu, naye huyu hapa askofu aliyefanya jambo lile lile, dhabihu saba safi, na pia kondoo dume saba, ikinena juu ya imani ya kwamba Mwana wa Mungu, Mwana-Kondoo wa Mungu, alikuwa yuaja.

83 Nena kuhusu mambo ya kimsingi, yeye ni wa kimsingi tu kama Israeli walivyokuwa, bali hakuwa na Roho, hakuwa katika ushirika na Mungu. Kama ndivyo ilivyo, Mungu hana budi kuwajibikia mambo ya kimsingi, basi bila shaka Yeye alimkataa mtu asiyefaa, mbona, ingembidi kuwakubali Moabu, na ilimbidi kuwakubali Israeli pia. Kama Mungu huchukua tu ibada, kanisa, madhabahu, Kaini alikuwa wa kimsingi tu kama Habili alivyokuwa, Kaini alijenga madhabahu, Kaini akatoa dhabihu, Kaini akaabudu. Madhabahu, kujiunga na kanisa, dhabihu, kanuni ya imani, na mambo haya yote, kama hayo ndiyo yote Mungu anayohitaji, alikosea wakati alipomhukumu Kaini, kwa sababu Kaini alikuja kwa njia ile ile aliyokuja nayo Habili. Kweli kabisa.

84 Lakini ilikuwa ni kitu gani? Kwa ufunuo, kwa ufunuo, si kwa elimu, bali kwa ufunuo. Habili aliona ya kwamba haikuwa ndizi wala matofaa, aliyokula Hawa, naye akatoa damu, ndipo Mungu akaikubali. Ilifunuliwa kwake.

85 Hiyo ndiyo sababu Yesu alisema, Mwenyewe, wakati aliposhuka kwenye Mlima wa Kugeuka Sura, alisema, "Ninyi mwasema mimi ni nani?"

86 "Mmoja akasema, 'Musa, Eliya,' na kadhalika." Mambo ya kimbinguni huchochea mambo kama hayo. Lakini Petro akasema, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai." Ile. . .

87 Naye akasema, "Heri wewe, Simoni, mwana wa Yona, mwili na damu havikukufunulia hili. Hukujifunza jambo hilo katika seminari, halikuwa Neno tu kwa jumla. Lakini Baba Yangu aliye Mbinguni, amekufunulia hili."

88 Sasa, kanisa Katoliki lilisema walijenga kanisa juu ya Petro, Waprotestanti walisema ilikuwa juu ya Kristo, nionavyo mimi, haikuwa hata mmoja. Ilikuwa ni juu ya ufunuo wa Neno, kwa kuwa Yeye alisema, "Wewe ndiwe Petro, wala mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu, aliye Mbinguni, amekufunulia. Na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu; na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda." Itaonyesha ya kwamba lango lote la kuzimu litakuwa dhidi Yake, bali kamwe halitashinda, Neno litaendelea moja kwa moja vivyo hivyo. "Juu ya mwamba huu ninalijenga Kanisa Langu." Ikionyesha ya kwamba kila kitu kitakuwa dhidi Yake, bali haliwezi kushinda, litaendelea moja kwa moja vivyo hivyo.

89 Sasa, maji ya farakano, yakitutenganisha, yakituruhusu kutambua ya kwamba sisi ni wenye dhambi, ya kwamba sisi ni wakosaji. Hiyo ndiyo sababu ningeweza kukishambulia kitu hicho, hiyo ndiyo sababu mhudumu yeyote anapaswa kupinga chochote ambacho Mungu anasema ni kosa kufanya. Akiwa amejazwa na Roho atafanya hivyo, kwa kuwa linatoka Mbinguni, mnaona, dhidi ya mabaya, hupaswi kufanya hivyo. Hayo ndiyo maji ya farakano.

90 Bado hiyo haikutosha, alifahamu, hayo yalikuwa ni maarifa yake, nia yake, tumbo la uzazi la nia yake, uwanja wa vita ambapo vita vinapiganwa, niani. Ndipo anaitupa kando, anaikubali kwamba ni njia ya Mungu iliyoandaliwa. Je, yeye yuko tayari kwa ajili ya ushirika sasa? La, la. Huo ulikuwa ni Ujumbe wa Luther. Moja kwa moja akaja . . . Yeye anaenda, anaelekea katika njia nzuri sasa. Anaelekea njia gani? Kuelekea kwenye kusanyiko. Huyu hapa ametengwa *hapa*, kwa maji, kuoshwa kwa maji ya Neno, ametenganishwa na dhambi yake.

91 Sasa, yeye anageuka, ndipo hana budi kutambua ile milia saba. Laiti tungalikuwa na wakati wa kuingilia jambo hilo, nyakati saba za kanisa, vinara vya taa saba, vivyo hivyo, kila—kila wakati, kila kanisa, kila kitu kingine, hakina budi kutambua ni Damu, kila mwaminio. Angali ndani, si katika ushirika, kusanyiko liko ndani likiabudu, bali yeye yuko hapa nje akijiweka tayari. Angali anabishania madhehebu na mashirika, kila kitu kingine.

92 Lakini anapoingia chini ya damu, anafanya nini alipoiangalia damu hiyo? Inatambua, inamfanya atambue ya kwamba kitu fulani kilikufa na kumwaga damu yake, kisha kikamtangulia kufanya njia kwa ajili ya ushirika. Kisha anaona milia ya damu mlangoni, anatambua, baada ya kujua Neno la Mungu, ndipo anakuja kutambua damu iliyomwagika. Naye hana budi kuja chini ya damu iliyomwagika, kama vile Israeli huko Misri na kadhalika, anakuja chini ya damu. Ndipo baada ya kujitambua . . .

93 Na Waebrania 13:12 na 13 ilisema, "Yesu, ili awatakase

watu kwa Damu Yake Mwenyewe, aliteswa nje ya malango." Yeye alikuwa Dhabihu yetu, kila elementi iliyotoka katika mwili Wake hufanyiza kuzaliwa upya.

94 Sikilizeni, enyi dada, mimi ni ndugu yenu, nami natumaini mnanielewa. Mtoto mchanga anapozaliwa, utaratibu wa kawaida wa kuzaliwa kwa kawaida ni upi? Jambo la kwanza, kama ni kuzaliwa kwa kawaida, ni maji, kinachofuata ni damu, halafu ni uhai. Kutoka katika mwili wa Yesu Kristo, walimchoma ubavuni: maji, Damu, kisha "mikononi Mwako naiweka Roho Yangu." Kulikuwa na elementi tatu zilizotoka kwenye Damu Yake: kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, hiyo inakupitisha kwenye Damu ukaingia katika ushirika.

95 Ndipo wakati mtu huyu, aliyetengwa na Neno, akatakaswa kwa Damu, anapoingia katika ushirika wa Kiungu, basi yuko katika kusanyiko la watu ambapo nguvu za Mungu zinashuka. Nao ushirika, hawajali nini *hiki*, *kile*, ama *kinginecho*, wote wako chini ya mahali pamoja na nia moja, "na Damu ya Yesu Kristo ikitusafisha na udhalimu wote," basi tuna ushirika sisi kwa sisi. Amina. Loo, jinsi ningeweza, tungeweza kushikilia hilo kwa muda kidogo! Naam, bwana.

96 Lakini hii hapa sababu, hiyo ndiyo sababu napenda mikutano hii ya Wafanyabiashara. Mtu fulani alipiga kelele si muda mrefu uliopita kwamba Wafanyabiashara watafanya, wajiunge na madhehebu fulani. Nikasema, "Watakapofanya hivyo, nitarejesha kadi yangu ya ushirika." Hilo linaliua papo hapo, linaua kila wakati, hakika linaua. Naam, bwana.

97 La, bwana, niko pamoja nao kwa sababu wanatetea kitu kile kile ninachoamini. Sijali kama wewe ni Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri, chochote ulicho, unapokuja chini ya hiyo Damu, ndugu, tuna ushirika sisi kwa sisi na kila mtu anaonekana sawa.

98 Wakati Yesu alipofundisha mfano huo maarufu, na kuzungumza juu ya karamu ya arusi: alimkuta mtu mmoja pale bila vazi la arusi. Ninyi. . . Tunajua desturi za watu wa mashariki, nimekuwa kule na ninajua kile. . . Wanatoa mialiko, na kila mtu aliye na mwaliko huja, awe maskini, awe tajiri, awe anaweza kuvalia vizuri ama hawezi, kuna mtu anayesimama mlangoni na, bwana arusi, na kumpa joho. Anapoingia, anavalishwa joho, sijali kama amevaa matambara, chochote alicho, anavaa joho, na kila mmoja wao wanafanana, kwa sababu wako chini ya joho, nao hawawezi kupata joho bila mwaliko.

99 Naye mtu huyu alikuwa ameingia kisiri kwa njia nyingine, asingeweza kuwa na ushirika kwa kuwa hakuwa amevalia sawasawa. Na wakati mtu anaporuhusu kanuni zake za imani ama dhehebu lake kumtenganisha na ndugu yake, kuna kasoro. Aliingia kisiri kupitia lango fulani la kimadhehebu, ama kitu

kama hicho, nayo Biblia ilisema, “Mfungeni, mkamtupe katika giza la nje, ambako kutakuwa na kulia, kuomboleza, kusaga meno.”

100 Ndugu, si kanuni za imani zinazotuingiza ndani, si kanuni za imani zinazoleta ushirika wetu. Ni . . . Elimu inatupeleka mbali sana nao kuliko kitu kingine chochote nijuacho. Mungu . . . Haikuwa mipango ya elimu, ilikuwa ni mpango wa kifo cha Mwanawe, kifo, kuzikwa, na kufufuka, kumwagwa kwa Damu, na kupitia hiyo, chini ya Damu hiyo, sote tuna ushirika sisi kwa sisi, huku Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, inatusafisha na dhambi yote.

101 Dhambi ni nini? Kutokuamini. Amina. Hakuna mtu katika ushirika huo ama ibada atakayepinga Neno lolote Mungu alilowahi kunena. Kwa nini? Dhabihu ile ile iliyomfia Ndiyo iliyoliandika Neno.

102 Katika Agano la Kale, wakati mwaminio alipokuja kuabudu, alikuwa amefanya kosa, asingeweza, isipokuwa aje kwa damu. Alifanya nini? Alimleta mwana-kondoo wake, akamwendea kuhani, kuhani akamchunguza huyo mwana-kondoo aone kama alikuwa ni mwana-kondoo mzuri, mkamilifu. Kisha akaweka mikono yake juu ya huyo mwana-kondoo na kukiri dhambi zake, ndipo dhambi zikahamishwa kutoka kwake hadi kwa huyo mwana-kondoo. Huyo nwana-kondoo hana budi kufa, kwa sababu yeye si mwenye dhambi tena, bali ni mwana-kondoo. Wakakata koo lake, damu ikamwagika, ikanyunyizia, ikateketea motoni. Vema.

103 Angalieni, sasa, hilo lingekuwa zuri vya kutosha. Lakini kwa nini, kwa nini hilo halikufanya kazi? Ilikuwa ikionyesha ya kwamba Kitu fulani kikubwa zaidi kinakuja, kwa sababu damu ya mbuzi au kondoo isingeweza kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi. Ingeweza kuifunika, bali isingeweza kuiondolea mbali. Kwa nini? Roho ambayo ndiyo uhai ulio katika hiyo seli ya damu, katika kemia ya damu, katika ule uhai, katika hiyo seli ya damu kulikuwa na uhai wa kondoo, naye kondoo huyo aliyekufa, uhai wa kondoo huyo usingeweza kumrudia mwabuduo, kwa hiyo usingefanya kazi.

104 Lakini tunapokuja Kalvari, kwa imani tuweke mikono yetu juu ya Mwana-Kondoo wa Mungu, nayo Seli ya Damu Yake ilivunjwa, ambayo haikuwa Myahudi wala Mmataifa, Yeye alikuwa ni Mungu, nasi, juu ya Damu hiyo isiyoghoshiwa, si kwa kujuana kimwili, bali kwa tendo la uumbaji la Yehova, Mwenyewe, Yeye aliyeumba ile Chembechembe ya Damu katika tumbo la uzazi la bikira na kumzaa Mwana wa Mungu . . .

105 Yeye hakuwa Mwana wa Mariamu. La, ita . . . Ninyi Wakatoliki mnamwita, “mama wa Mungu,” ati mnamwita. “Mama wa Mungu”? Yeye hata hakumwita “Mama” wakati mmoja, Yeye alimwita “Mwanamke,” hivyo ndivyo alivyokuwa.

Alikuwa ni kiangulio ambacho Mungu alitumia, kama tu vile Yeye angeweza kumtumia mtu mwingine yeyote. Yeye hakuwa "mama wa Mungu," Mungu hana mama. Yeye alikuwa Mungu peke yake, "Ndani Yake mlikaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili."

106 Tunapoweka mikono yetu pale na kukiri ya kwamba Yeye ni Mwokozi wetu na Mungu wetu, na wakati tunapoweka mikono yetu juu Yake kwa imani, na ile Damu iliyomwagwa pale Kalvari, tunaingizwa katika ushirika, naye Roho Mtakatifu aliyekuwa katika Seli hiyo ya Damu anamrudia mwaminio, akimfanya mwana ama binti wa Mungu, basi tuna ushirika. Na kama Roho Mtakatifu aliandika Biblia, Roho Mtakatifu anawezaje kamwe, chini ya Damu ambayo umeikubali, kurudi na kulikana Neno? Amina. Huo hapo ushirika, chini ya Damu. Amina.

107 Hilo ni safi kadiri niijuavyo Injili, ndugu. Huo ndio wokovu pekee niujuao, huo ndio pekee, ambapo imani yangu imejengwa, papo hapo, huo kwa Yesu Kristo, "Mishipa ya Imanueli, ambapo wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya gharika hiyo, hupoteza mawaa yao yote ya hatia." Ndipo tunapoingia kwenye hiyo, chini ya hiyo Damu na kujitambua wenyewe wenye dhambi, na kutokea ng'ambo ya pili, Naye anatia muhuri imani yetu namna hiyo, kwa Roho Wake Mtakatifu, Roho Mtakatifu yeye yule aliyeiandika Biblia na kuweka kila Neno ndani Yake, huyo Roho Mtakatifu anawezaje kugeuka na kulikana Neno hilo? Anawezaje kukubali kanuni ya imani badala ya Neno? Anawezaje kukubali fundisho la sharti badala ya Neno? Hawezi. Roho Mtakatifu ataitikia kila Neno la Mungu kwa, "Amina!"

108 Loo, jamani. Huo ndio ushirika ninaoamini. Basi si kwamba tu mna ushirika ninyi kwa ninyi, tuna ushirika pamoja na Kristo. Kwa nini? Sisi, tunajihesabu kuwa tumekufa, na kuzikwa, na kufufuka pamoja Naye katika ufufuo, na tumeketi katika ulimwengu wa Roho sasa katika Kristo Yesu.

109 Nilisoma hadithi ndogo si muda mrefu uliopita, katika kufunga, kulikuwa na mvulana wa Kimarekani, yapata kundi zima lao, walioenda Rumi kusomea sanaa, majumba mashuhuri ya sanaa ya Rumi. Uliwahi kuwa kule, ajabu sana! Ni wangapi wamewahi kuwa Rumi? Nadhani wengi wenu mmekuwako. Ulikuwa huko St. Angelo? Je, hilo halikukufanya ujionee aibu? Niliposhukia huko St. Angelo kuingia, mahali palipodhibitiwa na Katoliki, kulikuwa na bango kubwa, huko Rumi, ambapo kuna ukahaba, loo, *tsk*, lakini bango kubwa pale lilisema, "Kwa wanawake wote wa Marekani: Tafadhali vaeni nguo mkawaheshimu wafu." Hiyo ni Marekani yetu ya Kikristo, inaibidi Rumi kusema jambo kama hilo.

110 Vema. Katika nchi hii ya Rumi kulikuwa na msanii kijana, naye mzee mwangalizi wa mahali hapo akamwona huyu

msanii mchanga akiwa tofauti. Wote usiku, wanafanya kama wafanyavyo hapa.

111 Kwenye chuo *fulani* kikubwa cha Biblia hivi majuzi, tulikuwa tunakuja, tukienda kuvua samaki, nasi tukashuka kwenda mahali fulani kwa ajili ya kuvua samaki alasiri. Tukarudi juu, sijawahi kusikia kelele kama hizo maishani mwangu, wasichana wadogo kutoka kwenye chuo hiki maarufu, na wavulana wadogo, wamevaa kaptura, huko chini, loo, jamani, na mazungumzo usiowahi kuyasikia. Wakiburudika, hiyo, nafikiri walidhani hiyo ilikuwa ndiyo njia ya kufanya hivyo.

112 Wanawatoa wahudumu wa aina gani? Kizazi kijacho kitakuwaje? Kama kimejaa akina Ricky na Elvis sasa, ingekuwaje katika kizazi kingine? Itakuwaje? Haya basi. Loo, ndugu, hilo tu, kitu fulani kinaingia ndani yangu, siwezi kujizuia.

113 Angalieni, kijana huyu, alikuwa tofauti. Huyo mzee mwangalizi alimfuata siku moja. Kila siku angepanda kuelekea machweo ya jua juu ya kilima, na kuangalia kutua kwa jua, hasa, angeangalia ng'ambo ya nchi, akisimama pale huku ameweka mikono yake namna *hiyo*. Nao hao vijana wengine wote wangetoka baada ya shughuli za siku hiyo kwisha nao wangekunywa na kufanya yasiyofaa, baadhi yao wanakuwa na kuoga mchanganyiko, na karamu na kila kitu, wakipiga makelele, lakini kijana huyu...Siku moja...huyo mzee msimamizi, alimwangalia kila siku, alisumbuka sana kumhusu, kwa hiyo siku moja alipanda akamfuata, hapo karibu, huyo kijana alikuwa amesimama pale akiangalia ng'ambo ya pili ya bahari, kuelekea kwenye taifa hili, kuelekea machweo ya jua, huyo mzee mwangalizi akasema, "Samahani, Kijana Mwanamume, ningetaka kukuuliza swali."

Kasema, "Naam, Bwana. Ni kitu gani, Bwana?"

114 Kasema, "Sasa, umekuwa hapa zaidi ya mwaka mmoja," kisha kasema, "Nimekuangalia kila siku. Unakuja hapa juu yapata machweo wakati shughuli zimekwisha huko chini, masomo ye—yenu ya sanaa," kisha kasema, "unakuja hapa na kuangalia jua likitua." Akasema, "Mimi—mimi ni mzee anayetaka tu kujua," akasema, "Ni—ningetaka tu kujua ni kwa nini unafanya hivyo. Ni—ninataka tu kujua, labda, nina hamu tu ya kujua." Kasema, "Samahani kama nimekosea," kasema, "kwa kukuuliza."

Kasema, "La. La, bwana." Akasema, "Kwanza kabisa, mimi ni Mkristo."

115 Yule mzee msimamizi akasema, "Na mimi pia." Akasema, "Hilo linaniambia ni kwa nini huendi kwenye karamu, hutoki nje na kutenda kama hao wengine, hujihusishi nao." Kasema, "Ninaelewa hilo sasa, kwa kuwa wewe ni Mkristo," kasema,

"kwa kuwa nami ndivyo nilivyo." Akasema, "Ninaitazamia faraja ya kuja kwa Bwana."

116 Kwa hiyo wakisimama pale pamoja, huyo kijana alikuwa amenyosha mkono na kumkumbatia huyo baba mzee, akamkumbatia na kumvuta karibu naye, kasema, "Umeoa?"

Kasema, "Naam, nimelea kundi kubwa la watoto."

117 Akasema, "Bwana, sababu ya mimi kuangalia huko, ninaomba." Akasema, "Unajua, huko mbali nchini Marekani, kuna jimbo *fulani* katika hiyo Marekani kubwa, na katika jimbo hilo kuna mji *fulani*, na katika mji huo *fulani* kuna nyumba *fulani*, na katika nyumba hiyo kuna msichana, yeye ni Mkristo, pia, na unaona," akasema, "jua linapokuja hapa, liko mahali tofauti kule, bali tuliweka nadhiri kwamba tungeangalia wakati Mungu akilipitisha jua." Kisha kasema, "Niliahidi ya kwamba ningeishi mwaminifu kwake, yeye aliahidi angeishi mwaminifu kwangu kote maishani." Kisha kasema, "Siku moja ninatarajia kwenda kwake na kumfanya bibi-arusi wangu." Kasema, "Hiyo ndiyo sababu ninajaribu kuishi jinsi ninavyoishi, kwa sababu nimefanya ahadi, nami ninataka kuwa mwaminifu kwa ahadi yangu."

118 Loo, kama sisi siku hizi kama Wakristo, tunaokiri kuwa Wakristo, laiti tungeweza kujitenga na kila kitu cha ulimwengu, kanuni zetu zote za imani na kadhalika, na kusimama kuelekea, tutazame Mbinguni, tukijitenga na mambo ya ulimwengu na kuishi kama Wakristo kwa sababu siku moja, kuna Mahali *fulani* panapoitwa Mbinguni, "Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi," siku moja Yeye anakuja kwa ajili yetu, na hebu tuwe wakweli na waaminifu hata wakati huo. Na njia pekee tutakayoweza kufanya hivyo, enyi marafiki, ni wakati tunapozaliwa mara ya pili, wala hatuwezi kuzaliwa mara ya pili mpaka tuingie chini ya Damu iliyomwagika ya Yesu Kristo.

119 Katika kufunga mkutano huu, ningetaka kuchukua nafasi hii pamoja nanyi, marafiki, marafiki zangu, ndugu na dada zangu, natumaini mtaniruhusu niwe ndugu na dada yenu. Natumaini ninaweza kuwa kwenu kama—kama rafiki halisi, ninyi dada mnaweza kuwa dada yangu, ninyi ndugu, ndugu yangu. Je, ninaweza kuwa mchungaji wenu? Je, ninaweza kuwa mmoja wa raia wenzenu wa Ufalme wa Mungu nikiabudu pamoja nanyi?

120 Hebu na tuchukue nafasi hii na kusema hivi: Yote tuliyosikia, leo, rafiki yangu mwema, Ndugu David duPlessis, walisema, amehubiri saa tatu ama nne leo, ndugu mwingine nisiyemjua, alisema, "Jamaa mdogo alihubiri asubuhi ya leo," siku baada ya hiyo, Ndugu Brown, mhubiri mashuhuri, ndugu mashuhuri, ndiyo kwanza aingie njiani, zile jumbe kuu ambazo mmesikia kutoka kwa hao ndugu, hebu tusiziache tu zipitie juu yetu. Hebu tusifanye hivyo. Hebu na tutembee chini ya Damu ya Bwana

Yesu, usiku wa leo. Hebu na tujiweke wakfu upya kwa Mungu mwishoni mwa ibada hii, usiku wa leo, na kusema, “Bwana Yesu, nichukue. Niweke chini ya Damu Yako, na jalia nikuone Wewe pekee, Bwana, na unijalie nikuabudu Wewe.”

121 Rudini kwenye kanisa mnalotoka, kwenye dhehebu mnalotoka, lakini kumbukeni, unapokutana na ndugu au dada aliye katika dhehebu lingine, kamwe usijitenge, yeye ni ndugu yako, huyo ni dada yako, nyote mko chini ya Damu ya Bwana Yesu Kristo. Hivi huwezi kufanya hivyo?

122 Je, ungetaka kuyaweka wakfu maisha yako upya, usiku wa leo? Ningependa kuwaulizeni. Jana usiku (nawapenda kwa hilo.), baada ya kuwakemea sana, vikali, basi nilitoka nje na kupangusa machozi kutoka machoni mwangu kwa kulazimika kusema hayo, bali sina budi kutii yale niliyoambiwa niseme, ningeweza tu kufanya hivyo, nikatoka nje. Na hata hapa ambapo ninadhani ya kwamba karibu yapata kundi kubwa la watu hawa walikuwa ni Wapentekoste, lakini wakati Neno lilipotoka kwenye maadili na mambo ya kanisa siku hizi, nilisema, “Ni wangapi wenu mnaojitambua mmekosea, na mngetaka kuingia katika ushirika huu wa Kristo?” Na yapata asilimia tisini na tano ya kusanyiko, wakiwa na imani halisi ya Kikristo ya kutosha, pamoja na uaminifu wa kutosha moyoni mwako kutaka kutenda mema, uliinua mkono wako moja kwa moja mbele ya jirani yako na ulitaka kukumbukwa katika maombi. Nina imani kwenu, ninaamini ya kwamba Mungu atalijalia.

123 Sasa, si lazima iwe ni wakati fulani wowote, wakati wowote uliowekwa, inaweza kuwa ni wakati huu, wakati ukiwa tayari na uko radhi kukutana na Mungu juu ya msingi wa Neno Lake na kusema, “Mungu, nifinyange na unifanye kwa mtindo Wako Mwenyewe.” Kama utafanya hivyo, usiku wa leo, katika ibada ya kuweka wakfu, kabla tu hatujafunga, ninaamini Mungu atakutana na kila mmoja wenu. Na kama sitawaona tena upande huu wa mto, nitawaona kwenye Ng’ambo ya pili, mkiamini Neno lile lile, pamoja na Ujumbe ule ule, ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Lake halitashindwa kamwe. Unaamini hilo?

124 Je, uta—utajiunga pamoja nami katika kujiweka wakfu? “Nitajiunga, ninataka niwe katika kuweka wakfu kuyaweka wakfu tena maisha yangu kwa utumishi wa Mwenyezi Mungu. Jalia nisikate tamaa kamwe. Jalia nidumu mkweli na mwaminifu na kulihubiri Neno.” Je, ungetaka, ungetaka kuwa Mkristo wa namna hiyo? Ni wangapi wangetaka kuwa Mkristo halisi, na kuninii tu, vema, Mkristo kamili? Inueni mikono yenu. Sasa, kuwa tu mwaminifu, Mkristo halisi? Mungu awabariki. Hebu na tusimame kwa miguu yetu.

125 Loo, jamani. Huu ndio wakati, sasa ndio wakati. Loo, laiti—laiti ningalijua la kusema, na ningalilisema, kama

ningalijua la kusema. Unamaanisha hilo? Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote alionipa Baba watakuja kwangu." Ni kitu gani kilichokufanya usimame kwa miguu yako? Hivi kweli ulimaanisha tuliyosema? "Niko tayari kuyaweka wakfu maisha yangu?" Je, uko tayari kujifia mwenyewe na kila kitu kinachokuzunguka, hakuna kitu ila Damu ya Yesu Kristo ndiyo yote unayotamani?

Ni kitu gani kinachoweza kuosha dhambi yangu?
Hakuna ila Damu yake Yesu;
Ni kitu gani kinachoweza kunifanya mzima tena?
Hakuna ila Damu yake Yesu.

126 Hapo una ushirika pamoja na Kristo, pamoja na Mungu, pamoja na Malaika, pamoja na Roho Mtakatifu, pamoja na viumbe vyote vya Mbinguni, na viumbe vyote vya duniani, kwa sababu mwili wote Mbinguni na duniani unaitwa kwa jina Lake. Hiyo ni kweli. Nanyi ni familia moja kubwa mno, mtakuwa na ushirika mmoja na mwingine. Na tumwinulie Mungu mikono yetu sasa, na kwa wimbo wetu wa kujiweka wakfu:

Nampenda, nampenda
kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

[Ndugu Branham anavumisha, *Nampenda*—Mh.] Fungeni tu macho yenu sasa. Sasa huku mioyo yenu imeinamishwa:

Nampenda (Hilo ni Neno Lake.), nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Juu . . .

Iweni tu kama mtoto mdogo sasa, rahisi, mkikiri.

Na-. . .

Utamu Wake, uingie mioyoni mwetu, Roho Mtakatifu.

Kwani alinipenda kwanza

Rahisi sasa. Mkubali tu aingie ndani. Ihifadhi nafsi yangu, Bwana.

. . . wokovu . . .

(*Imani Yangu Inakutegemea Wewe.*)

. . . Kalvari . . .

127 Sasa hebu na tuinamishe mioyo yetu na vichwa vyetu kwa muda kidogo tu. Jiweke wakfu kwa Mungu sasa. Kwa utulivu, kwa njia yako mwenyewe, omba maombi yako, "Na, Mungu, nichukue sasa, ninasimama katika Uwepo Wako. Mkutano huu umemaanisha mengi sana kwangu. Nichukue, Ee Mungu. Ondoa

jiwe moyoni mwangu. Siku moja sina budi kuondoka, Bwana, huenda ikawa ni usiku wa leo, sijui itakuwa ni lini, bali na—nataka kukupenda Wewe, Bwana Yesu. Ninataka kuwa Wako."

Imani yangu inakutegemea Wewe,

Omba tu hilo huku ukiimba.

Ewe Mwana-Kondoo wa Kalvari;
Mwokozi wa Kiungu;
Sasa nisikie ninapoomba,
Ondolea mbali dhambi zangu zote,
Ee nijalie kuanzia leo,
Kuwa Wako kabisa!

128 Sasa huku vichwa vyenu vimeinamishwa, na kinanda kikiendelea kucheza, sasa, usijiweke wakfu nusu tu, wazia tu sasa unaposhuka chini: "Ondoa kwangu, Bwana, yote yasiyofanana Nawe. Nijalie niwe mtoto Wako, tangu wakati huu na kuendelea." [Ndugu Branham anavumisha—Mh.] Sasa unapoendelea mbele zaidi:

Huku nikitembea duniani kwenye mzingile wenye giza,
Na huzuni zimenizunguka,
Uwe Kiongozi wangu;
Agiza giza ligeuke kuwa mchana,
Futilia mbali hofu za huzuni,
Wala usiniache nipotee kamwe
Kutoka Kwako kwenda kando.

129 Baba wa Mbinguni, utamu wa Roho, utamu wa muziki, uwe Kiongozi wetu, Bwana, kila mmoja wetu kwa njia zetu mbalimbali, ukijua udhaifu wetu, Bwana, nasi tunaziungama Kwako, tukiomba ya kwamba utatusamehe, Ee Mungu. Tupeleke katika nyumba ya Mfinyanzi, usiku wa leo, utuoshe katika Damu ya Bwana Yesu, na kutufinyanga kwa hiyo Kemikali ndani yetu, Bwana, ili kwamba unapotutazama tutakuwa weupe kabisa, kwa kuwa tunaikubali Damu ya Bwana Yesu.

130 Tunaomba ya kwamba utajifunua Mwenyewe kwetu, Bwana, katika Neno. Tunajua ya kwamba huu ni mpango Wako, Baba. *Hili* ni nanii Wako—*Hili* ni Nabii Wako, Neno ni Nabii, Linatabiri, chochote kinyume Chake kingekuwa ni kutomtii huyo Nabii, Biblia.

131 Nasi tunaomba, Bwana, ya kwamba utatuvunjavunja, usiku wa leo, mioyo yetu ya mawe, njia zetu za mawe, na kutuumba na kutufinyanga katika mfano wa Mwana wa Mungu, kwa Damu Yake Mwenyewe, kusudi ushirika wetu daima uweze kuwa mtamu na mkuu.

132 Mungu, jalia kwamba ubariki kanisa hili kuu linalomiliki uwanja huu, ambalo limeturuhusu kuja hapa, hili Shirika la Kibaptisti la Marekani lililoufungua, na wakaifungua milango

yao tupate kuingia hapa kama watu wa Full Gospel. Ninaomba Mungu, ya kwamba kutakuwa na uamsho wa mtindo wa kale utakaoibuka miongoni mwao, kwamba Roho Mtakatifu atamwagwa kwenye kila mnara wa maombi, na kote katika misitu hii watajaa watakatifu, wakiimba, na kusifu, na kupaza sauti, ishara kuu na maajabu na yaje miongoni mwao, Bwana, wao ni ndugu zetu, tunawaombea.

133 Tunaomba kwa ajili ya kila kanisa na kila shirika, kila dhehebu, kwamba watavunja pingu hizo na kamba, na kukimbilia Mwambani. Tujalie, Bwana. Saa imekaribia sasa tunapomtazamia Yeye kuja, wakati tunapomwona mwanamwali aliyelala akianza kutamani Mafuta. Ndipo walipoenda kuyanunua, Bwana-arusi akaja, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Na, Bwana, tunaiona ikiwa karibu sana sasa.

134 Tunaomba, Bwana, ya kwamba utatujalia kuamka upesi sana, taa zetu zitengenezwe na kuwaka. Makanisa yameanza kutambua ya kwamba yalikosa kitu Fulani. Nasi tunaomba, Baba, sasa kwa kuwa wanakitafuta, kwamba tutajiweka tayari. Hivyo ndivyo Wewe ulivyosema, "Basi walipokuwa wameenda kununua Mafuta, ndipo Bwana-arusi akaja." Tusaidie, Mungu Mpendwa.

135 Tunayaweka wakfu maisha yetu Kwako. Na kama vile nimewaomba ndugu zangu na dada zangu hapa kufanya hivyo, mimi mwenyewe ninafanya, Ee Mungu, ninajilaza juu ya Mwamba, kama yule tai niliyenena habari zake jana usiku, Ee Mungu, kwa kila maombi nijuayo, niondolee kila kitu kiovu, Bwana. Ninaomba ya kwamba Wewe utanifinyanga mpaka uninii, ni—niweze kuyaakisi Maisha Yako. Tujalie, Bwana. Nisaidie kuwa mkweli na mwaminifu, nisaidie daima kuwa na nguvu na jasiri, nisaidie, Baba, kulipeleka Neno kwenye nchi zisizofanyiwa umishenari za ulimwengu. Tujalie, Baba.

136 Bariki Shirika hili la Wafanyabiashara, na liishi, na jalia lifanikiwe, na kuendelea, na kukuona kuja kwa Bwana, na kuwaweka watu wengi tayari. Watu wenye heshima, watu waadilifu, watu walio mashuhuri, wanaotumia riziki zao wenyewe, wanachukua wakati wao, kuleta Injili, kuwasaidia wahudumu kuingia na kulieneza Neno, Mungu, tunawapenda, nasi tunaomba ya kwamba watakuwa na nguvu nchini, na kutumiwa mkononi Mwako.

137 Mbariki kila mhudumu aliye hapa. Mbariki Ndugu yetu Brown, Ndugu yetu duPlessis, na ndugu wengine wote, Ndugu Joseph Boze, na wengine wote, wafanyabiashara, na wote pamoja, Bwana. Na kila dada, bariki mioyo yao, Baba, tunaomba ya kwamba Wewe utakuwa pamoja nao. Na utusamehe dhambi zetu zote. Nasi tunajiweka wakfu Kwako sasa, kama watoto Wako, tangu leo na kuendelea jalia tuishi maisha tofauti.

Tunaomba, katika Jina la Yesu, tunapojikabidhi mikononi Mwako, fanya nasi upendavyo. Amina.

138 Mnaweza kuketi sasa kwa muda kidogo tu. Nampenda. Hivi hamumpendi? Mnajisikia vizuri zaidi sasa? Hivi Neno haliwasugui sana, na kuwafanya tu mjisikie mmeburudika kabisa na kila kitu? Ni ajabu. Tunampenda Bwana kwa moyo wetu wote. Hivi hamumpendi? Vema.

139 Sasa, nitairudisha ibada kwa Ndugu Carlson hapa, nadhani, ndugu yetu, mwenyekiti, naye atakuja na kuchukua ibada sasa.

140 Kama tukikusanyika mwaka mmoja kuanzia leo, nami niishi, hawa labda wataninii . . . Huenda nisiishi mwaka mmoja kuanzia leo, huenda Yesu akaja kabla haujafika, lakini ikitokea nirudi kwenye mmoja wa mikutano mingine hapa, ule mkutano wa mkoa wa jimbo hili kuu, kutakuwa na baadhi yetu watakaokosekana. Tuna hakika kabisa na jambo hilo, na umri wetu, na jinsi mambo yanavyoendelea, idadi iliyo hapa. Na kama sitawaona tena mpaka nitakapokutana nanyi mtoni, Mungu awabariki na awe pamoja nanyi mpaka wakati huo. Mungu akubariki, Ndugu Carlson.

141 [Ndugu Carlson anafanya kusanyiko limwombee Ndugu Branham—Mh.] Bwana akubariki, Ndugu. Asanteni, marafiki. Asante, Baba. Ninayapokea, Bwana. Na—najua ya kwamba utayasikia hayo maombi, naamini utayasikia. Tujalie, Bwana. Nisaidie sasa. Ee Mungu, jalia Neno liwe, nishikilie sasa. Jalia liwe parokia yangu, na jalia niwe mshiriki wa baraka Zako, Bwana. Ninakushukuru kwa ajili ya watu hawa waungwana . . . ? . . . Ninapokea na kuamini maombi yao. Katika Jina la Yesu. Amina. [Ndugu fulani anaomba—Mh.] Tujalie, Bwana. Amina. Jina la Bwana lisifiwe.

142 Asante, ndugu yangu Mkristo. Marafiki zangu Wakristo huko nje, nitaninii, nitategemea hayo. Ninaenda sasa hudumani, mnajua ninakoenda. Nikirudi tu, ninaenda, ninakusudia kukutana na Ndugu yetu Boze huko Afrika mara moja, kupitia Afrika na sehemu mbalimbali za ulimwengu. Nitakuwa nikizikumbuka baraka zenu zote pamoja nami nina hakika. Niombeeni nami nitaendelea kuwaombea. Mungu awe pamoja nanyi.

Asante, Ndugu.

62-0519 Ushirika
American Baptist Assembly
Green Lake, Wisconsin Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org